

DAWA MIZIZI MIREFU

Maradhi yameenea, Kaskazini yajia
Wanyama wayachukua, ndio watutawanyia
Fisi mbweha nasikia, ni wenye kutuletea
 Maradhi si malaria, yamezidi hata wehu.

Hayajawahi tokea, waganga hawajajua
Wamechunguza kwa nia, waganga nawasifia
Ila hawakugundua, ugonjwa unavyokua
 Hili gonjwa la ajabu, mtaalam ni nani?

Watatu walijifia, waganga kuangalia
Dalili kujionea, vidudu vikitembea
Mganga vikamwingia, kesho yake kajifia
 Daktari Kariuki, Mungu amweke pema.

Hofu ikatuingia, ugonjwa umenuia
Sisi sote kutuua, taifa ladidimia
Wengine walikimbia, ati kujiondokea
 Ugonjwa waleta baa, nchi ipo mashakani.

Waganga kuendelea, mabuku kujisomea
Machweo ilitokea, lakini kwa kukisia
Ukiitwa Kefilia, ni ugonjwa wa hisia
 Mawazo yakawazonga, huku umeingiae?

Mabuku kuyapekua, wanyama kuwapasua
Uchunguzi kutimia, waganga kupambanua
Wadudu wenye mikia, ndio wanaotuua
 Wadudu baakokai, ndilo jina walopata.

Tiba wakafikiria, waganga walosomea
Tabu ikawaingia, jinsi ya kuwaua
Sumu walizqtumia, wadudu wavumilia
 Dawa gani watumie, watu wasishambuliwe?

Waganga wakapania, wadudu kuwatimua
Misitu wakaingia, madawa kuyachimbua
Mizizi waliing'oa, ila haikuwajia
 Akili zikawakuna, kama upele wa ngozi.

Siku zikajiendea, na watu wakaugua
Wengine walijifia, bahati ikatokea
Dawa ikasadidia, ikatuliza hisia
 Dawa hiyo kitulizo, si dawa ya kuponyesha.

Waganga huendelea, nia haijakimbia
Lakini hii hisia, wazee yawasumbua
Dawa haijakolea, vidudu vyawazoea
 Baakokai wagumu, dawa mizizi mirefu.